ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

2019/20

GAVANA
BENKI KUU YA TANZANIA

Juni 2019

ISSN 0856-6976

MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

2019/20

GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA

Juni 2019

Utangulizi

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, Benki Kuu inatoa Tamko la Sera ya Fedha linaloweka bayana mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2019/20. Tamko hili linajumuisha mapitio ya mwenendo wa uchumi na utekelezaji wa sera ya fedha ya mwaka 2018/19, na kuainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2019/20 yanayoendana na mahitaji ya malengo mapana ya kiuchumi ya Serikali ya kusimamia utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi. Tamko hili pia linaelezea hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa na Benki Kuu ili kufikia malengo hayo.

Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Kulingana na taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Aprili 2019, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2018, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2017. Ukuaji mdogo wa uchumi wa dunia ulichangiwa zaidi na athari za kiuchumi kutokana na majanga ya asili yaliyoikumba Japan, kuongezeka kwa vikwazo vya kibiashara baina ya Marekani na China, kudorora kwa upatikanaji wa rasilimali fedha, na kutokutabirika kwa athari za Uingereza kujitoa kwenye Umoja wa Kiuchumi wa Nchi za Ulaya.

Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea ulifikia asilimia 2.2 mwaka 2018, ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.4 kwa mwaka 2017. Hali hiyo ilichangiwa zaidi na kupungua uzalishaji wa magari nchini Ujerumani kutokana na kuanza matumizi ya sheria mpya za uchafuzi wa mazingira; kudorora kwa uwekezaji nchini Italia; na kupungua kwa matumizi ya

walaji nchini Ufaransa. Ukuaji wa uchumi nchini Uingereza ulipungua na kufikia asilimia 1.4 kutoka asilimia 1.8, hasa kwa sababu ya hofu ya kujitoa kutoka katika Jumuiya ya Ulaya (Brexit). Nchini Japan, ukuaji wa uchumi ulipungua hadi asilimia 0.8 kutoka asilimia 1.7, kutokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi katika robo ya tatu ya mwaka 2018, kulikosababishwa na hali mbaya ya hewa na maafa. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi nchini Marekani umebakia kuwa imara, ukikua kwa asilimia 2.9 mwaka 2018, ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2017, ingawa kumekuwa na kusuasua kwenye uwekezaji katika nusu ya pili ya mwaka 2018.

Ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua ulifikia asilimia 4.5 mwaka 2018 ukilinganishwa na asilimia 4.8 mwaka 2017. Ukuaji huu ulisababishwa na kudorora kwa masoko ya fedha katika nusu ya pili ya mwaka 2018. Ukuaji wa uchumi nchini China ulipungua hadi asilimia 6.6 mwaka 2018 kutoka asilimia 6.8 mwaka 2017, ukichangiwa zaidi na kupungua uwekezaji wa ndani, kupungua kwa mauzo ya magari pamoja na mvutano wa kibiashara na Marekani. Ukuaji wa uchumi nchini India ulikuwa asilimia 7.1 mwaka 2018, ukilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2017. Ukuaji wa uchumi wa nchi za kusini mwa jangwa la Sahara umeendelea kuimarika katika mwaka 2018, japo kwa kasi ya chini, huku wastani wa Pato Halisi la Taifa ukikadiriwa kukua kwa asilimia 3.0 mwaka 2018, kutoka asilimia 2.8 iliyofikiwa mwaka 2017.

Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) mwezi Aprili 2019, inakadiria uchumi wa dunia utakua kwa asilimia 3.3 mwaka 2019, kutokana na matarajio ya ukuaji mdogo wa uchumi katika nchi zilizoendelea. Ukuaji wa uchumi

wa mataifa yaliyoendelea unakadiriwa kupungua na kufikia asilimia 1.8 mwaka 2019, kutokana na kuendelea kwa mvutano wa kibiashara baina ya China na Marekani, hofu ya nchi ya Uingereza kujitoa kutoka katika Jumuiya ya Ulaya (Brexit), na makadirio ya ukuaji mdogo wa uchumi wa nchi katika bara la Ulaya kutokana na kudorora kwa mahitaji ya sekta binafsi na uzalishaji viwandani. Ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua, unatarajiwa kukua chini ya asilimia 5.0 mwaka 2019, kutokana na kupungua kwa ukuaji wa uchumi wa China, na kudorora kwa uchumi wa Uturuki na Iran. Wakati huo huo, inakadiriwa kuwa ukuaji wa uchumi wa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara, utaongezeka na kufikia asilimia 3.5 mwaka 2019 kutoka asilimia 3.0 mwaka 2018, kutokana na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji uchumi kunakochangiwa zaidi na uwekezaji katika miundombinu.

Viwango vya mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi vimeendelea kubaki katika viwango vya chini kutokana na kushuka kwa bei za chakula na nishati. Katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), kasi ya mfumuko wa bei umeendelea kubakia katika kiwango kilichokubaliwa cha chini ya asilimia 8.0 kutokana na upatikanaji mzuri wa chakula. Katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), wastani wa mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia asilimia 11.9 mwezi Aprili 2019 kutoka asilimia 8.5 mwezi Aprili 2018, ukichangiwa zaidi na kupanda kwa bei za chakula, mavazi na gharama za usafirishaji.

Kulingana na taarifa ya mwelekeo wa hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Aprili 2019, viwango

vya mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2019, kutoka asilimia 2.0 mwaka 2018 kutokana na matarajio ya kupungua kwa bei za bidhaa. Wakati huohuo, mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi na zile zinazoendelea kukua unatarajiwa kuongezeka kidogo hadi kufikia wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2019, kutoka asilimia 4.8 mwaka 2018; kutokana na matarajio ya kuimarika kwa mahitaji nchini India na kupanda kwa bei za vyakula kwenye baadhi ya nchi.

Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

Tanzania Bara

Uchumi wa Tanzania umeendelea kukua kwa kasi ya juu, ambapo kwa mwaka 2018[1] uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.8 na asilimia 6.9 kwa mwaka 2017 na 2016, kwa mpangilio huo. Ukuaji huu umechochewa zaidi na uwekezaji katika huduma za kijamii na miundombinu, kutengemaa kwa ugavi wa umeme, hali nzuri ya hewa na utekelezaji wa sera ya fedha ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na sanaa, burudani na starehe; ujenzi; usafirishaji na uhifadhi; sayansi na teknolojia; na mawasiliano. Shughuli za ujenzi zimeendelea kuwa na mchango mkubwa kwenye ukuaji wa uchumi zikifuatiwa na usafirishaji na uhifadhi, mazao na viwanda. Uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.1 mwaka 2019, kufuatia uwekezaji unaoendelea katika kuboresha miundombinu na huduma za jamii, upatikanaji wa uhakika wa umeme, kuimarika kwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi, na uzalishaji

1 Kizio cha mwaka 2015

viwandani. Matarajio ya ukuaji wa juu wa uchumi yatatokana pia na maboresho yanayofanywa na serikali katika sheria na kanuni mbalimbali, mageuzi ya sera katika kujenga mazingira ya kuongeza uwazi katika kufanya biashara, pamoja na mkakati wa utekelezaji wa sera ya viwanda.

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, mfumuko wa bei umeendelea kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0, na ndani ya vigezo vya muunganiko wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) usiozidi asilimia 8.0, na wigo uliokubalika katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya asilimia 3.0 na 7.0. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini, utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na kibajeti, na kutengemaa kwa uzalishaji na ugavi wa umeme. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.2 ikilinganishwa na asilimia 4.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati ulikuwa wastani wa asilimia 2.7 ukilinganishwa na asilimia 1.6. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubakia ndani ya lengo la asilimia 5.0 katika mwaka 2019/20, kutokana na matarajio mazuri ya upatikanaji wa chakula cha kutosha, kuendelea kutengemaa kwa usambazaji wa umeme na utekelezaji thabiti wa sera ya fedha na kibajeti.

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti za Serikali zilizoko Benki Kuu ya Tanzania yalikuwa shilingi bilioni 14,690.4, ikiwa ni asilimia 3.4 zaidi ya mapato yaliyokusanywa na kuwekwa kwenye akaunti hizo katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 93.1 ya makadirio ya makusanyo katika kipindi hicho. Mwenendo huu wa makusanyo ya

mapato kwa sehemu kubwa umetokana na jitihada zinazotekelezwa na Serikali katika kuongeza matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji wa kodi kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na kuongezeka kwa jitihada za usimamizi wa ukusanyaji wa mapato. Katika kipindi hicho, jumla ya matumizi ya Serikali yaliyofanywa kupitia katika akaunti zake zilizoko Benki Kuu yalifikia shilingi bilioni 16,363.6 kati ya hizo shughuli za maendeleo ziligharimu shilingi bilioni 4,864.6.

Urari wa malipo nje ya nchi (*balance of payments*) ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,089.2 katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 299.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*). Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 2,132.6 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,709.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18 kufuatia kuongezeka kwa thamani ya bidhaa za mitaji zilizoagizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya miradi mikubwa ya maendeleo, hasa ya miundombinu. Nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje inatarajiwa kufikia asilimia 4.4 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19, kutoka asilimia 3.5 mwaka 2017/18.

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha na kuendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2019, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 4,395.2, kutoka

kiasi cha dola za Marekani milioni 5,188.0 mwezi Aprili 2018 na dola za Marekani milioni 5,483.9 mwezi June 2018. Kiasi hicho kinatosha kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.3, ambacho ni juu ya lengo la nchi la kukidhi miezi isiyopungua minne. Rasilimali za fedha za kigeni za benki za biashara zilikuwa dola za Marekani milioni 1,031.4 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2019.

Deni la Taifa limeendelea kuwa himilivu, japokuwa liliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 22,981.3 mwezi Aprili 2019, kutoka dola za Marekani milioni 21,976.8 mwishoni mwa mwezi Aprili 2018 na dola za Marekani milioni 22,760.4 mwezi Juni 2018; ambapo asilimia 71.8 ya deni hilo lilikuwa ni deni la nje. Aidha, kwa mwaka unaoishia mwezi Aprili 2019, deni la nje linalojumuisha deni la serikali na la sekta binafsi, liliongezeka kwa asilimia 7.8 hadi kufikia dola za Marekani milioni 21,587.9. Wakati huo huo, deni la ndani limeongezeka kwa asilimia 3.3 na kufikia shilingi bilioni 14,844.1. Hati fungani zimeendelea kuwa sehemu kubwa ya deni la ndani ikiwa ni sawa na asilimia 68.0 ya deni lote mwishoni mwa mwezi Aprili 2019, kama ilivyokuwa mwishoni mwa mwezi Aprili 2018.

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka April 2019, sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha inayowiana na viwango vya kisheria. Uwiano wa mtaji wa msingi wa sekta ya kibenki ukilinganishwa na jumla ya rasilimali ilikuwa asilimia 17.0 mwishoni mwa mwezi Aprili 2019, ikilinganishwa na kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10.0. Aidha, uwiano wa ukwasi ulikuwa asilimia 33.6, ikilinganishwa na kima cha chini cha kisheria cha asilimia 20.0. Vilevile,

uwiano wa mikopo chechefu kwenye mikopo yote ulikuwa asilimia 11.1 mwezi Aprili 2019 kutoka asilimia 11.6 mwezi Aprili 2018, kiwango ambacho bado kipo juu ya lengo la Benki Kuu la asilimia 5.0. Benki Kuu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha sekta ya kibenki hasa katika kupunguza uwiano wa mikopo chechefu; baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuhimiza benki na taasisi za fedha kutumia kanzi data ya taarifa ya historia za wakopaji (*credit reference bureau information system*) kabla ya utoaji wa mikopo mipya, ili kupunguza uwiano wa mikopo chechefu na kusaidia kuongeza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi yenye riba nafuu.

Aidha, Benki Kuu imeendelea kusimamia kanuni na miongozo katika kuimarisha udhibiti wa vihatarishi katika sekta ya fedha, ikiwa ni pamoja na miongozo kwa Wakurugenzi wa benki na taasisi za fedha. Benki Kuu pia imeendelea kupitia vigezo vipya vya Basel II/III na kuchambua kulingana na mahitaji ya vigezo hivyo kwenye mitaji ya benki na utoshelevu wa ukwasi.

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi na kuendelea kuongezeka kwa matumizi ya kidigitali katika utoaji wa huduma za kifedha. Kuanzia mwezi Julai 2018, malipo yote ya serikali yalianza kufanyika kupitia mfumo wa Akaunti Moja ya Hazina (*Treasury Single Account*, TSA) na kutumia mfumo wa kielektroniki wa kuhamisha fedha kutoka katika akaunti ya benki moja hadi nyingine (*Tanzania Automated Clearing House,* TACH), na mfumo wa malipo wa Benki Kuu ya Tanzania (*Tanzania Interbank Settlement System,* TISS) kwa miamala ya zaidi ya shilingi milioni 10.

Matumizi ya mifumo hii ya malipo imewezesha serikali kuongeza ufanisi katika malipo na kupunguza gharama zinazoambatana na malipo kupitia hundi. Aidha, mfumo wa malipo wa Afrika ya Mashariki (*East Africa Payment System,* EAPS) uliendelea kufanya kazi kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa miamala ndani ya mfumo huo hali inayoashiria ongezeko la shughuli za kiuchumi baina ya Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aidha, utoaji wa huduma za kifedha baina ya mitandao ya simu kupitia simu za mikononi umeendelea kuongezeka kwa kasi katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019. Katika kipindi hicho, miamala inayotumia simu za mikononi iliongezeka na kufikia milioni 145.5, ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 4,886.4, sawa na ongezeko la asilimia 81.6 ikilinganishwa na miamala iliyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18; na ongezeko la asilimia 47.7 ikilinganishwa na thamani iliyopatikana katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hadi kufikia mwezi April 2019, Watanzania wapatao milioni 22.4 walikuwa watumiaji wa miamala kwenye mfumo wa malipo kupitia simu za mikononi, ikilinganishwa na Watanzania milioni 20.1 na milioni 20.6 waliokuwepo mwishoni mwa mwezi Aprili na Juni 2018, kwa mtiririko huo.

Zanzibar

Uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika, ukikua kwa wastani wa asilimia 6.3 katika kipindi cha mwaka 2011 na 2018. Katika mwaka 2018, Pato la Taifa la Zanzibar lilikua kwa asilimia 7.1, likilinganishwa na asilimia 7.7 mwaka 2017. Shughuli zilizochangia kwa kiasi kikubwa

ukuaji huo ni pamoja na shughuli za malazi na huduma ya chakula; biashara na matengenezo; na usafirishaji na uhifadhi. Ukuaji wa uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kuendelea kuimarika ambapo unategemewa kukua kwa asilimia 7.8 mwaka 2019, ukichangiwa zaidi na uwekezaji katika huduma za afya, elimu, miundombinu, na uwekezaji wa sekta binafsi katika shughuli za utalii.

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, mfumuko wa bei umepungua na kufikia wastani wa asilimia 3.4, kutoka asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hali hii ilichangiwa zaidi na kushuka kwa bei za vyakula hususan unga wa mahindi, ndizi na sukari, pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta. Aidha, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubakia katika viwango vya tarakimu moja kwa mwaka 2019/20, licha ya changamoto ya uwezekano wa kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, mapato ya ndani ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 637.0, sawa na asilimia 94.1 ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi hicho. Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato kumetokana na jitihada mahususi za kuongeza usimamizi wa ukusanyaji wa mapato zilizofanywa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) pamoja na Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB). Jumla ya matumizi yalikuwa shilingi bilioni 966.9; kati ya hizo, matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 372.5.

Urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 51.6 katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 28.2

katika kipindi kama hicho mwaka 2017/18. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za nje, hususan mafuta na chakula pamoja na kupungua kwa mauzo ya karafuu nje ya nchi.

Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2018/19

Malengo ya Sera ya Fedha

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kuhakikisha uwepo wa kiwango cha kutosha cha ukwasi kwenye uchumi unaoendana na malengo ya uchumi mpana, ikiwamo utulivu wa mfumuko wa bei na ukuaji wa shughuli za uchumi; pamoja na utulivu wa riba katika masoko ya fedha. Ili kufikia malengo ya Serikali ya uchumi mpana kwa mwaka 2018/19, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim wa asilimia 11.5;
ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 12.2;
iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 10.2; na
iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa Mwaka 2018/19

Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Aprili 2019, Benki Kuu iliendeleza utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi katika mazingira ya utulivu wa mfumuko wa bei. Msimamo huu wa sera ya fedha ulilenga kuziwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza kasi ya

utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kukuza shughuli mbalimbali za uchumi. Hivyo basi, Benki Kuu ilipunguza riba ya mikopo kwa mabenki (*discount rate*) kutoka asilimia 9.0 hadi asilimia 7.0 mwezi Agosti 2018, pamoja na kuendelea kutumia zana za sera ya fedha kuongeza ukwasi ikiwamo: kununua fedha za kigeni, na kuendelea kutoa mikopo ya muda mfupi kwa mabenki. Hatua hizi zimesaidia kuboresha hali ya ukwasi kwenye sekta ya benki pamoja na kusaidia utulivu wa riba katika masoko ya fedha. Riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki (*overnight interbank cash market rate*) kwa mwezi Aprili 2019 ilikuwa asilimia 5.20 ikilinganishwa na asilimia 1.69 mwezi Juni 2018 na asilimia 1.29 mwezi Aprili 2018. Ongezeko hili la riba linaashiria ongezeko la mahitaji ya ukwasi wa shilingi kwenye mabenki kufuatia kuendelea kuimarika kwa utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Vilevile riba za dhamana za serikali zilikuwa wastani wa asilimia 8.20 mwezi Aprili 2019 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.59 mwezi Juni 2018 na wastani wa asilimia 4.04 mwezi Aprili 2018.

Katika kipindi cha Julai 2018 mpaka Aprili 2019, wastani wa riba za mikopo inayotolewa na mabenki imeendelea kupungua japo kwa kasi ndogo na kufikia asilimia 17.15, wakati riba za amana zilikuwa wastani wa asilimia 7.65. Hali hii inaashiria kupungua kwa tahadhari inayowekwa na mabenki ikihusisha matumizi ya kanzi data katika uidhinishaji wa mikopo, pamoja na marekebisho yanayoendelea kufanywa kwenye miongozo na kanuni mbalimbali za usimamizi wa sekta ya fedha nchini.

Aidha, mfumo wa kielektoniki wa soko la fedha baina ya mabenki ulianza kufanya kazi rasmi mwezi Machi 2019, na benki zote zimeanza kutumia mfumo huo katika kufanya miamala. Mfumo huu unasaidia upatikanaji

wa viashiria halisi vya ukwasi kwenye mabenki na hatimaye kusaidia usimamizi wa utekelezaji wa sera ya fedha na uhalisia wa riba katika masoko ya fedha. Wakati huo huo, Benki Kuu ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa mwongozo wa makubaliano ya uendeshaji wa soko la mikopo ya muda mfupi baina ya mabenki kwa kuweka dhamana (*Global Master Repurchase Agreement*) ambao ni muhimu katika utekelezaji wa sera ya fedha.

Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) umeendelea kukua kwa wastani, wakati ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ukiendelea kuimarika kwa kasi. Ukuaji wa mwaka wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulifikia asilimia 4.9 mwezi Aprili 2019 ambao ni chini ya lengo la asilimia 12.2 kwa mwaka unaoishia mwezi Juni 2019. Ukuaji huu wa fedha unaakisi ongezeko la matumizi ya kielektroniki katika kufanya malipo, hali ambayo imeongeza kasi ya mzunguko wa fedha katika shughuli za uchumi. Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua na kufikia asilimia 10.6 mwezi Aprili 2019, kiwango ambacho ni cha juu kuwahi kutokea tangu mwezi Oktoba 2016 na juu ya lengo la ukuaji wa asilimia 10.2 ifikapo Juni 2019. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unaenda sambamba na muendelezo wa utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi, pamoja na hatua zinazochukuliwa katika kupunguza mikopo chechefu kwenye benki za biashara kulikotokana na matumizi ya kanzi data ya taarifa za wakopaji katika kuidhinisha mikopo.

Thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu mbalimbali duniani imeendelea kuwa tulivu kwa kipindi chote cha kuanzia mwezi Julai 2018 mpaka Aprili 2019, japo kulikuwa na mabadiliko ya juu kiasi mwezi Januari na Februari 2019. Mabadiliko hayo yalitokana zaidi kwa kuwa kipindi

hicho ni msimu wa mapato madogo yatokanayo na mauzo ya mazao nje ya nchi na shughuli za utalii, sambamba na ongezeko la uagizaji wa bidhaa za mitaji kutoka nje ya nchi kwa ajili ya miradi mikubwa ya maendeleo.

Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2019/20

Katika mwaka 2019/20, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zitaendelea kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (*Second Five Year Development Plan 2016/17 – 2020/21*) na Mpango wa Kukuza Uchumi Zanzibar (*MKUZA III 2015-2020*) zinazolenga kuendeleza jitihada za kuweka misingi imara ya uendelezaji wa viwanda na kukuza uchumi shirikishi kama hatua ya kuufikisha uchumi wa nchi kuwa wa kipato cha kati. Katika mwaka 2019/20, Serikali zinalenga yafuatayo:

i. Ukuaji wa Pato la Halisi Taifa la asilimia 7.1 kwa Tanzania Bara kwa mwaka 2019;

ii. Mfumuko wa bei ulio ndani ya kiwango cha tarakimu moja; na

iii. Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada kutoka nje (*grants*) ya asilimia 2.3 ya Pato la Taifa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mwaka 2019/20.

Kwa upande wa Zanzibar, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa asilimia 7.8 mwaka 2019, wakati nakisi ya bajeti ya serikali ya Zanzibar inatarajiwa kuwa asilimia 3.9 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20.

Ili kufikia malengo ya Serikali ya uchumi mpana kwa mwaka 2019/20, Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga

kuimarisha utulivu wa bei pamoja na utulivu wa riba katika masoko ya fedha. Kwa mwaka 2019/20, Benki Kuu imepanga kufikia malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslim wa asilimia 9.0;

ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.0;

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 13.5; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Benki Kuu itaendelea kuboresha ufanisi wa masoko ya fedha kuendana na mabadiliko ya utekelezaji wa sera ya fedha itakayotumia riba ya Benki Kuu. Vile vile, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha kwa uwazi na kwa kutumia zana mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa kiasi cha ukwasi kwenye benki za biashara kinabakia katika kiwango kinachoendana na mahitaji ya wakati huo, na hivyo kuleta utulivu wa riba katika soko la fedha baina ya mabenki.

Hitimisho

Uchumi wa Tanzania unatarajia kuendelea kuwa imara kutokana na jitihada za Serikali katika kuendelea na uwekezaji katika huduma za jamii na miundombinu chini ya awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango wa Kukuza Uchumi Zanzibar. Miradi inayotekelezwa katika mipango hii ni chachu katika kukuza sekta binafsi na kuwezesha uchumi wa viwanda. Kuendelea kuimarika kwa kasi ya ukuaji wa mikopo

kwa sekta binafsi kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi katika uchumi, kuongezeka kwa uzalishaji viwandani pamoja na maboresho ya kanuni, sheria na sera zinazolenga mageuzi ya uchumi wa viwanda yatachangia katika ongezeko la Pato la Taifa katika mwaka 2019/20. Hata hivyo, athari zinazotokana na kuongezeka kwa vikwazo vya kibiashara baina ya mataifa makubwa duniani zinaweza kuathiri ukuaji wa uchumi wa Tanzania siku zijazo.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0 kutokana na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula; kuimarika upatikanaji wa nishati; na utekelezaji wa sera thabiti za fedha na kibajeti. Hata hivyo, kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia pamoja na hali ngumu ya upatikanaji rasilimali fedha katika soko la dunia kunaweza kuathiri thamani ya shilingi ya Tanzania na hivyo kusababisha mfumuko wa bei.

Benki Kuu itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa uchumi wa dunia na wa nchi katika kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kudumisha utulivu wa mfumuko wa bei, na kuchukua hatua kulingana na uwiano wa sera na mikakati ya nchi katika kukuza uchumi. Hivyo, kutokana na tathmini ya mwelekeo wa uchumi wa dunia na uchumi wa ndani, pamoja na sera zinazotarajiwa kutekelezwa, ni matarajio ya Benki Kuu kuwa malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2019/20 yatafikiwa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz